**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**

# TANGAZO LA ZABUNI

**TAREHE 02/01/2026**

Kamati ya maendeleo ya Wilaya (CDC), inayosimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kwa ushirikiano wa kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi na Shirika la CAMFED inawaalika wafanyabiashara mbalimbali wenye uwezo wa kutoa huduma na vifaa vinavyohitajika kushiriki katika mchakato wa kuidhinisha kwa ajili ya kutoa huduma hizo kwa mwaka 2026/2028. Watoa huduma watakaopitishwa kupitia mchakato huu wataingizwa kwenye orodha ya wazabuni watakaoshindanishwa wakati wa manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali zinazohitajika katika utekelezaji wa mradi.

Tangazo hili linawahusu watu binafsi, kampuni, vikundi au Taasisi zote zilizosajiliwa kisheria na zenye uwezo wa kutoa huduma au bidhaa husika kulingana na mahitaji ya miradi ya maendeleo.

Vifaa na huduma zinazohitajika vimeorodheshwa katika jedwali hapo chini,

| NA. | VIFAA / HUDUMA | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Malazi-Malazi na Huduma za mikutano Hotel na nyumba za wageni | Hoteli, Hostel nk. |
| 2 | Huduma za chakula na vinywaji | Kwenye mikutano mbalimbali watu 30 nk. |

**Zingatio.**

**Waombaji wote wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:**

1. Kujaza fomu ya kuomba kuwa mzabuni inayopatikana katika ofis ya Afisa Elimu wa Wilaya -Sekondari na kuambatanisha Pamoja na barua ya maombi. Fomu hii inatolewa BURE.
2. Muombaji awe na uzoefu wa kufanya kazi na Taasisi za Serikali ama Taasisi zisizo za kiserikali (NGOs) na aorodheshe taasisi ambazo umefanya nazo kazi miaka ya karibuni

CamScanner

3. Muombaji awasilishe maombi kwa Afisa Elimu wa Wilaya- Sekondari S.L.P 70 ITIGI au Ofisi ya CAMFED Wilaya akiambatisha:
   i) Nakala ya uhalali wa kisheria ( power of Attonery) kwa muombaji ambae ni kampuni.
   ii) Nakala ya vyeti vya usajili wa kampuni/Ushirika/Vikundi
   iii) Nakala ya uthibitisho wa ulipaji kodi yam waka 2025 (Tax clearence) cheti cha VAT, TIN na leseni halali ya Biashara au huduma husika.
   iv) Taarifa za banki ( Jina la account nan amba ya account).
4. Maombi yatapokelewa kuanzia Tarehe 07/01/2026 mpaka tarehe 18/01/2026. Maombi yote yatakayotumwa baada ya tarehe hizo hayatapokelewa.
5. Mwombaji anaruhusiwa kuomba kutoa huduma/kusambaza bidhaa zaidi ya moja kati ya zilizoainishwa ikiwa ana vielelezo vya kuthibitisha kufanya biashara husika na kila huduma iombwe tufauti
6. Kila ombi lijazwe vizuri na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (plain), ifungwe kwa nakiri , (SEALED) na juu ya bahasha iandikwe **MAOMBI YA KUWA MTOA HUDUMA- CDC.**
7. Muombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima
8. Watoa huduma watakaochaguliwa watajulishwa kwa barua na watatakiwa kujaza fomu ya maadili ( code of conducts) na kuzirudisha kwa Afisa Elimu – Wilaya/ Mwenyekiti wa CDC.
9. Watoa huduma wasiochaguliwa watajulishwa kwa barua pia.
10. Waombaji wote wawe ndani ya Mkoa husika.

**N.B; Maombi yote yatumwe kwa mwenyekiti wa CDC ambaye ni Afisa Elimu wa Sekondari wa Halmashauri.**

IMETOLEWA NA

[signature]

**K.n.y <u>MKURUGENZI MTENDAJI (W)</u>**

**<u>HALMASHAURI YA ITIGI</u>**

K.n.y: MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

CamScanner